


Je yeote ameshaw ahi kukuonyesha kutoka
kwa Biblia jinsi unavyo weza kujuu kwa
hakika kuwa utaenda Mbinguni Ukifa?



Neno Injili inamaanisha habari njema. Ni habari njema jinsi unavyoweza kuwa na uhusiano wa upendo na wa kibinafsi na Mungu iletayo maana na makusudi kwa haya maisha na pia ikupatie hakikisho ya kukaa milele na Mungu kule Mbinguni.

Watu wengi leo husema kuwa wana hubiri injili ilhali ujumbe wao huwa tofauti.



Mbona sisi husikia ujumbe tofauti tofauti leo? Je kuna Injili zaidi ya moja? Injili hasa ni nini, Kulingana na Bibilia?

Copyright © 1988 by Ronald R. Shea.
All Rights Reserved

Kabla hatujaanza, ungeweza kujibu maswali haya matatu yenye umuhimu?

1. Je, umewahi kuambiwa injili ni nini?

2. Ukifa usiku wa leo na usimame mbele ya mungu na kisha akuulize "Mbona nikiruhusu uingie katika mbingu yangu?" Un gesemaje?

3. Ukifa sasa hivi, je unajua hakika kuwa utaenda mbinguni?

- Ndiyo! Bila shaka kwa hakika nitaenda mbinguni.
- La! Sina "uhakika kamili" kuwa nitaenda mbinguni.

DHAMBI


Kuelewa habari njema ya jinsi uhusiano kati ya Mungu na Binadamu inaweza kurejeshwa, mmoja lazima kwanza mtu aelewe jinsi uhusiano huo ulivyoharibika.

Neno la Mungu la tufunza:

Wote wametenda dhambi na kypungukīwa na utukufu wa Mungu. Warumi 3:23

Tulikufa dhambini . . . Waefeso 2:5

Mungu ni mtakatifu (msafi kiroho) na mwanadamu ni mwenye dhambi (mchafu kiroho). Jinsi mtu ambaye ni msafi kimwili hawezi kuvumilia kukaa karibu na mnyama aliyekufa, kuoza na kunuka ndivyo Mungu aliye mtakatifu na mkamilifu hawezi kuruhusu mwanadamu mwenye dhambi na asiye mkamilifu aingie katika uwepo wake. Mwanadamu amekufa katika dhambi zake!



Mwanadamu msafi
kimwili

KUTENGWA NA MUNGU

Matokeo ya dhambi ni dhahiri:

Dhambi zako zimeweka kizuiizi kati yako na Mungu wako. Isaya 59:2




Binadamu mwenye dhambi
(mchafu kiroho)

Mungu ni mtakatifu (msafi kiroho na hana mwisho) kwa hivyo Yeye ni mtakatifu bila kikomo! Basi hata dhambi ndogo zaidi inachukiza mno mbele Zake. Kwa hivyo Bibilia hufunza ya kwamba hata dhambi ndogo zaidi imetosha kumtenga milele binadamu na Mungu wake. Mungu hawezi kuruhusu dhambi uwepo Wake.

Jitihada za mwanadamu ni Bure!

Mwanadamu kila mara ametafuta njia kuvuka kizuizi ambacho kilichomtenga na Mungu, anajaribu kupenya kuititia ubatizo, matendo mema, kwa kumpenda jirani wake, sakramenti, kuungana na kanisa flani ama dhehebu n.k. Lakini Bibilia hufunza ya kwamba hakuna matendo ya mwenye dhambi ambayo yanaweza kupenya kizuizi cha dhambi ambacho humtenga Mungu mtakatifu na mwanadamu mwenye dhambi.



Bibilia inasema:

Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi. Isaya 64:6


Kujaribu kuacha dhambi zetu kuititia matendo yetu yenye ni kazi bure kama vile kuosha uso kwa kutumia kitambaa kichafu, hakika hakuna kitu chochote mwanadamu anaweza kufanya kufuta dhambi zake na apenye kizuizi kinachomtenga na Mungu. (Pia tazama. Haggai 2:12-14), Luka 18:10-14, Warumi 3:20; 3:27-38; 4-5, Wagalatia 3:10-11, 21)

Injili

Neno "Injili" maana yake ni Habari Njema, kwa vile hatuwezi kuingia katika uwepo was Mungu na dhambi zetu, Mungu alimtuma Yesu afe kwa ajili ya dhambi zetu na kumfufua kutoka wafu siku ya tatu.

Basi, ndungu zangu, nawaarifu ile injili... ya kuwa kristo Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko na kuwa alizikwa na kuwa alifufuka siku ya tatu; kama yanenavyo maandiko. 1 wakorintho 15:1-4

Mungu



Basi, Yesu alivunja kizuizi cha dhambi kwa kuzifia dhambi zetu na kufufuka kutoka mautini.

Watu wengi leo huamini kuwa Yesu alikufa na akafufuka kutoka mauti, lakini Bibilia inamaanisha nini ikitasema ati Yesu "alizifia dhambi zetu?" Kifo chake kilivunja aje kizuizi baina ya Mungu na Mwanadamu?

Tatitizo: Mungu lazima atawaadhibu wote wanaobeba hatia ya dhambi.

Bibilia inatuambia ya kwamba kwa vile Mungu ni mtakatifu na mwenye haki, lazima atawaadhibu wote wabebao hatia ya dhambi.

Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana; kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu imedhishirishwa huwajia wana wa uasi.. Waefeso 5:6

Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhishiriswa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovo wa wanadamu. Warumi 1:18



Mungu lazima
alete ghadhabu
yake juu ya
dhambi.

Haki ya Mungu inahitaji kwamba wote wabebao hatia ya dhambi lazima waadhibiwe na Mungu. (Wathesalonike wa pili 1:8-9, Mathayo 25:46, Ufunuo 20:10) Jinsi Kristo alivyotuweka huru kutoka kwa ghadhabu ya Mungu. Kupitia kwa kifo chake inaweza kuelezwaza kwa hatua tatu.

HATUA-YA 1: KUBEBA / KUCHUKUA Kristo alichukua dhambi zetu juu yake.

Hatua ya kwanza katika ukombozi wa mwanadamu ilikuwa ni Yesu Kristo abebe dhambi za dunia mwilini mwake pale msalabani. Yesu alipotundikwa msalabani, Mungu alichukua dhambi za ulimwengu wote (yaliyopita, yaliopo na yajao) na kumwekeea Kristo.

Na Bwana ameweeka juu yake maovu yetu sisi sote.

Isaya 53:6

Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti.

Petro 2:24

Yeye [Mungu Baba] asiyejua dhambi alimfanya [Yesu] kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu. Katika yeye 2 Wakoritho 5:21

KATIKA MAHAKAMA YA MBINGUNI YESU ALITANGAZWA KUWA NA HATIA YA DHAMBI ZA ULIMWENGU.



Kwa ajili Mungu lazima aadhibu wote waliobeba hatia ya dhambi, Nani ndiye sasa Mungu ata adhibu?

HATUA YA 2: MABADILIKO KRISTO ALIKUFA KWA NIABA YETU.

Kwa kuwa Mungu lazima awaadhibu wote wanaobeba haitia ya dhambi, aliwachilia ghadhabu yake juu ya Yesu badala yetu. Yesu aliadhibiwa badala yetu. Na akafa badala yetu.

Aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu na kufa kwa niaba yetu. Baši alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubusilwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake.

Isaya 53:5

Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema.. "Mungu wangu Mungu wangu, mbona umeniacha."

Mathayo 27:46



HATUA YA 3 : RIDHISHA (TULIZA)

KIFO CHA KRISTO ILILIPA DHAMBI ZETU ZOTE, KWA HIVYO KULITULIZA GHADHABU YA MUNGU NA HAKI. Tangu Yesu afe kwa niaba ya dhambi zetu, haki ya Mungu iliridhishwa. Yesu alilipa dhambi za wanadamu wote, kwa hivyo kwa mtu apekeaye malipo hii hatawai pitia ghadhabu ya milele ya Mungu ambayo inastahili kumpata kila mwenye dhambi.

Lakini Bwana aliridhika kumchubua; Amemhuzunisha. Utakapofanya (Mungu Baba) Nafsi yake (Yesu) kwa dhabibu kwa dhambi.. ataona mazao ya taabu ya nafsi yake na kuridhika.

Isaya 53:10-11

Basi Yesu alikwisha kuipokea ile siri alisema, "imekwisha." Akainamisha kichwa akai salimu roho yake.

Yohana 19:30

Yesu aliposulibwa msalabani alisema "Kimekwisha" kilitumika na warumi nyakati za Kiristo wakati deni lote lilikwisha kamilika kulipwa. Wakati Yesu alipiga kelele kabla ya kufa. Alikuwa akionyesha kuwa alikuwa amelipa kikamilifu ya mwisho ya dhambi. (Pia angalia wakolosai 2:13-14).



KWA HIVYO YESU ALIVUNJA KUZUIZI BAINA YA MUNGU NA BINADAMU KWA KULIPA DHAMBI ZETU KUPITIA KIFO CHAKE PALE MSALABANI.

Je, kufa kwa Yesu unaumuhimu. Itakuwaje kifo cha Yesu kiwe cha dhamana sana kiasi ya kwamba kinaweza kugharimia dhambi zetu zote na pia dhambi zote za wanadamu wa nyakati zote?

Yesu ni Mungu

Yesu ni Mungu. Milele ye ye hutoshana na Mungu baba kwa kila sehemu, alifanyika mwanadamu ili azifiye dhambi zetu wala hakukoma kuwa Mungu!

Tomaso akajibu, akamwambia, Bwana wangu na Mungu wangu, Yesu akamwambia, wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki, heri wale wasioniona, wakasadiki.” Yohana 20:28-29

Pia tazama Yohana 1:1, 8:58-59, fananisha na kutoka 3:13-14, Yohana 10:30, 1 Timotheo 3:16; Tito 2:13, Wakolosai 2:2, Waebrania 1:8)

Wale wanaokana Uungu wa Yesu watapokea hukumu ya milele. Yesu alisema:

Akawaambia, ninyi ni wa chini, mimi ni wa juu, ninyi ni wa ulimwengu huu.. mimi si wa ulimwengu huu. Kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba mtakuwa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu. Yohana 8:23-24

Pia tazama Yohana 11:25-27; 20:31, matendo ya mitume 9:20; 16:30-31; waraka wa kwanza wa Yohana 5:13.

MBONA MUNGU ALIFANYIKA MWANADAMU?

Katika uk.5 tulijifunza ya kwamba Mungu ni mtakatifu kabisa. Hata kiini kidogo sana cha dhambi kinamkwaza kabisa. Kwa hivyo malipo ya hali ya juu zaidi lazima ilipwe kwa ajili ya dhambi zetu. Basi tunazo njia mbili ambazo bei hii inaweza kulipwa, mwanadamu alijiona mwisho anaweza teseka chini ya ghadhabu ya Mungu kwa muda usio na kipimo, mwanadamu asiyе na mwisho anaweza kuteswa chini ya Mungu kwa muda fulani uliowekwa. Mambo haya mawili ni malipo ya juu sana kwa dhambi zetu.

1. Mwanadamu aliye na mwisho anaweza basi kuteseka chini ya ghadhabu ya Mungu kwa muda usio na mwisho. Ikiwa atataka kujilipa dhambi zake mwenyewe. Ndiposa Jahanamu ni ya milele.

2. Yesu kristo, Mungu asiyе na mwisho kataka umbo kama mwanadamu ilimbidi apitie ghadhabu ya Mungu kwa wakati uliopangwa. Kwa ajili ye ye ni Mungu mateso aliyoyavumilia msalabani ilikuwa yanastalihili kulipa dhambi za wanadamu wote wa nyakati zote.

Gharama isiyokuwa na mwisho lazima ilipwe kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote. Mungu uruhusu kila mtu a'amuе aina gani ya mpango wa malipo anayopenda kutumia . . . Yesu kristo au kukaa milele motoni.

IMANI: MWITIKO WA MWANADAMU KWA KRISTO

Yesu alifanya kazi yote iliyohitajika ili kumuokoa mwanadamu kutoka kwa dhambi zake. Hata hivyo kabla hatujatambua faida ambazo Mungu amepeana kupitia kifo cha Yesu msalabani, mungu anatuhitaji tumwamini (kumsadiki) Yesu, pamoja na yale aliyotimiza kupitia kwa kifo chake.


Hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu, wala si kwa matendo ya sheria, maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakaye hesabiwa haki.

Wagalatia 2:16

Kwa maana jinsi hii Mungu alisupenda ulimwengu ndiposa akamtoa mwanawewe wa pekee, kwani yule atakayemwamini hatakuwa bali atapokea uzima wa milele.

Wohana 3:16

(Kuna zaidi ya mistari mia moja sitini (160) katika agano jipya ambazo zinatangaza kwamba nji ya kupokea uzima wa milele ni imani katika Yesu Kristo. Mionganoni mwao ni (Yohana 1:7, 1:12, 3:18. 5:24, 6:29 n.k.)



Imani (kusadiki) ni mkono ule ambao tunanyosha na ku'ufikia uzima wa milele ipatikanayo bure ndani ya Yesu Kristo.

Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alisupenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa.

1 Wakorintho 1:21

NEEMA: KIPAWA CHA BURE

Hili neno "Neema" ina maanisha toleo la bure... bile gharama ukajaribu kumlipa kwa ajili yake, je bado unaweza kuliita zawadi? Bila shaka hapana. Inabadilika na kuwa deni ambalo anakudai kuanzia wakati alikubali pesa yako! Rafiki yako bila shaka anaweza kutukanya aregeshe zawadi na kusema: "sipeani hili kwako kwa ajili ninataka. Ni zawadi. Je unakubali zawadi yangu ama hapana?"

ZAWADI. WAKATI UNAPOPEA KITU ILIKUPOKEA NYINGINE SI ZAWADI TENA. INAKUWA DENI!



Lakini kwa mtu afanye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni. Warumi 4:4

Wakati tu utakaporejesha ujira (wako ufukoni mwako na kisha onyesha mkono wako mtupu hapo. Ndipo atakubali na kukupatia ile zawadi).

Vivyo hivyo ni kweli na jinsi Mungu anavyo na uzima wa milele. Watu hujaribu kununua uzima wa milele kwa kutii amri kumi, kuishi maisha mema, kuenda kanisani, ama kufanya kazi zengine za dini, lakini Mungu hatakubali kudaiwa na mwanadamu ye yeyote "hadaiwi" uziwa wa milele na yeyote. Atapeana tu kama zawadi!

NEEMA : LAZIMA IWE BURE

Wakati mwanadamu anajaribu kupokea uzima wa milele kuitia matendo yake mwenyewe, yeye tena hakubali zawadi ya uzima wa milele kutoka kwa Mungu kama zawadi ya bure, hiyo ndio, kwa "neema."

Au hapo neema isinge kuwa neema.

Warumi 11:6b

Iliali tunaokolewa tu kwa neema ya Mungu!

Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia nija ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha mun-gu, wala si kwa matendo, mtu awaye yote asiye akajisifu.

Waefeso 2:8-9

Kwa hivyo maandiko hufunza kuwa Mungu hutuo zawadi ya uzima wa milele kutoka kwa yeyote anayejaribu kuipata kuitia, kwa matendo yao na basi kumshusha Mungu kwa kumfanya kuwa mwenye deni wa mtenda dhambi.

Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakohesabiwa haki kwa she-ria mmeanguka na kutoka katika hali ya neemao.

Wagalatia 5:4



MUNGU HUPEANA UZIMA WA MILELE KAMA ZAWADI YA BURE NI LAZIMA KUIKUBALI KAMA ZAWADI YA BURE, AMA SIVYO KABISA .

Kwa hivyo kujaribu kupokea uzima wa milele kuitia kwa matendo ya sheria ni kukataa njia ya pekee ambayo Mungu ampeana nayo uzima wa milele, hiyo ni, kwa neema yake. Wakati mwanadamu anakataa toleo la Mungu la neema ya uzima wa milele, anakubali bila malipo hukumu ya milele.

TOBA: TOBA BILA SHAKA NDIYO NENO AMBALO LIMEKOSA KUELEWEKA VYEMA ZAIDI KATIKA LUGHA YA KINGEREZA.

KILE AMABACHO SI TOBA IOKOAYO:

1. Toba iokoayo sio kujihurumia kwa dhambi zako.
2. Toba iokoayo sio kugeukia dhambi zako au badilisha upya maisha yako.
3. Toba iokoayo sio kupeana maisha yako kwa Mungu kwa hiari ili aongeze njia zako. Neema iokoayo haina lolote. Kuhusiana na wewe kujuta kwa ajili ya dhambi zako au kuamua kutozirejelea tena. Mungu anahiari kuukoaka jinsi ulivyo tu. Biblia inasema.

*Baśi Mu aonyesha pendo ląkę yeye mwenyeww kwetu sisi
·
Warumi5:8*

Maana ya toba iokoayo:

Toba iokoayo ni kuacha kuamini kupata uzima wa milele kuititia dini, tamaduni za kidini au kufuata amri za Mungu.

Neno "toba" ni neno la ugiriki linalomaanisha "kubadili matendo maoni, wale wanaoamini kuwa uzima wa milele hupatwa kwa kufanya matendo mema wanaamriwa kuititia maandiko matakatifu kubadili maoni yao au "toba." Wanambiwa waache kuamini matendo yao, na kuja kwa Mungu kwa msingi wa neema kuititia imani pekee.

Mathayo 3:7-9: wanadini wengine waliamini kuwa wataenda mbinguni kwa sababu wao walitoka katika ukoo wa Ibrahimu, baba wa Wayahudi. Mungu mwenyewe alkagua wayahudi na kuanzisha dini yao. Watu hao waliamini kwa sababu walikuwa dini ya ukweli wangeenda mbinguni. Yohana mbatizaji aliwaambia lazima wa tubu. Hiyo ni, lazima waache kuamini katika dini yao kuenda mbinguni.

Luka 13:1-5: Yatueleza juu ya mnara uliokuwa. Yerusalem na kisha kuanguka na kuua watu 18. Wayahudi wali tafuta jibu la mkasa huu. Walijua kuwa Mungu angejua

Fikra za kindani na matendo ya binadamu mwengine. Kwa wakati ule, walifikiri watu 18, ndio watenda dhambi zaidi. Mnara wa Siloam uliwaangukia 18, watenda dhambi zaidi. Pale Yerusalem, Mungu angewakusanya pamoja wakati haupendao na mahali na kufanya hukumu yake takatifu. Hii ingemaanisha kuwa watenda dhambi zaidi peke yake wanastahili hukumu ya Mungu. Waliosalia Yerusalem. (Wale ambao hawakuangukiwa na mnara ulioanguka). Walikuwa wameishi maisha ya wazi kutosha kutostahili hukumu ya Mungu. Kuamini aina hii ya mawazo, lakini, ni kuamini kuwa wokuvu kupata kwa matendo ya sheria. Yesu aliwakanya wale walioamini hivi kuwa walitazama laana ya milele. Aliwamuru wa tubu. Kuacha matumaini ya kupata nafasi ya haki melele ya Mungu kuititia matendo ya sheria, na kuamini kwa Mungu pekee kwa wokuvu wao.

Waebrania 9:9-14. Bibilia inataja sakramenti au tamaduni za kidini kuwa njia ambazo wanadamu hujaribu kumfikia Mungu " Matendo yaliyokufa" sura chache hapo awali, mwandishi huyu anatwambia kuwa Waebrania 6:1 kuwa msingi wa imani ya mkristo ni toba kutoka kwa matendo yasiyokuwa na uhai na imani kwa Mungu. Hiyo ni kusema, mtu lazima aache kutumia "matendo yasiye na uhai" (K.V. tamaduni za kidini, sakramenti n.k) kabla ya kutenda imani ya kweli ndi ya Mungu.

Amri ya bibilia ni wazi kama mtu anaamini kuwa dini itampeleka mbinguni, lazima yeye ataubu. (Mathayo 3:7-9) kama anaamini kufuata amri za Mungu ni muhimu kumpela mbinguni, lazima atubu (Luka 13:1-5) kama anaamini kuwa kufanya tamaduni za kidini ama sakramende ili yamwokoe (Waebrania 6:1). Kama mtu kwenye ukurasa 14, lazima kipawa cha bure!

Kutumainia Yesu hakutakuokoa kama unaamini kuwa Yesu alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu, na pia kuamini kuwa lazima ubatizwe, kwenda kanisani, am kufuata amri kumi ili kukusaidia kwenda mbinguni. Hiwezi kumwongeza Yesu nani ya mahitaji mengi ulionayo yanayokupasa kufanya ama kuwa ili kuingia mbinguni. Lazima kukataa mambu hayo yote kuwa thamini ya kuokoa kwa hali yote na kuammini Yesu Kristo pekee yake..

TOBA IOKOAYO

Wokovu kupitia



Kama imani ndiyo mkono unaopokea wokuvui kupitia Yesu Kristo, toba ndiyo mkono husiokubali wokuvu kupitia njia yoyote.

Imani iokoayo haidhibitishi tu kufa kwa Yesu ni "Muhimu" lazima idhibitise kifo chake kimetosha! Kuwa kimetosha kulpia dhambi zako kando ya kuwa jitihada za binadamu na matendo mema, na ni zawadi ya bure ipoke-wayo tu kwa imani, na kando ya jitahada za mwanadamu au matendo mema (tazama wagalatia 2:21, 3:10-14, 5:1-5, Warumi 4:5).

Rejelea ukurasa wa 3. jibu lako lilikuwa nini kwa mbona Mungu akaruhusu mbinguni? Kama ulisema lazima ubatizwe, ishi maisha mazuri, ama kitu chochote isipokuwa kumwamini Yesu. Lazima utubu. Lazima uwache kuamini kwa mambo yote ya dini uliyofanya awali ama hapo baadaye na kuamini kristo peke yake.

La, hapana! Si hitaji mambo hayo yoote ilikuokoka

Kwa ufupisho:

Kwa sababu dhambi zinatenga mwanadamu kwa Mungu, kwa sababu Yesu alilipia dhambi zetu msalabani, mwanadamu anaweza kuwa na uhusiano na Mungu kupitia tu kwa Yesu Kristo.

Yesu akamwambia, Yesu akamwambia, mimi ndimi njia na kweli na uzima, mtu haji kwa baba, ila kwa njia ya mimi.

Yohana 14:6

A.

Yesu ni Mungu,



Wokouvu

(tangazwa: "kutokuwa na hatia" kupitia dhambi zako zote na kuhakikisha uzima wa milele mbinguni.)

IS GIVEN
FREELY TO
ANYONE
WHO

Wokovu kupitia



1. Tubu kutokana na matendo ya-siyo na uhai

2. Na amini



Hushaamini kuwa kuishi hadi kiwango Fulani cha uziri au kutenda tamaduni Fulani za kidini ni muhimu kwenda mbinguni?

Bado unaamini mambo hayo kukuokoa?

Wakati huu, kwa njia nzuri huijuayo, unaamini yale Yesu alifanya msalabani. Kwako kuwa yote utakayo hitaji kuosha dhambi zako na kuhakikisha makao mbinguni?

Ndio

La

UHAKIKA

Kama umeweka imani yako kwa Kristo pekee, na ungetakikana kufa leo usiku, unauhakika kuwa utaenda mbinguni?

Yesu alisema,

Amini, amini, niwaambia, yeye asiyekiyaye neon langu na kumwamni yeye aliyepeleka yuna uzima wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. Yohana 5:24

Amini, amini nawaambia: Yesu alikuwa na uhakika gain? (umesikia maneno ya Kristo kwenye ukurasa wa kijitabu hiki. Alisikiaye neon langu

Alisikiaye neon kangu... Umesikia maneno ya kristo kenyé kurasa za kijitabu hiki?

Kumwamini yeye aliyenipeleka... Unaamini kwa Mungu alimtuma Yesu afe kwa niaba yako?

Ana uzima wa milele... Je unasema kuwa uthalipokea hapo baadaye au u tayari nayo?

Wala haingii hukumuni... Je bibilia inasema "Labda hapana au lazima hapana."

Bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. Ni wakiti gain mtu anavuka kutoka mautini kuingia uzimani?

Kutokana na mstari huu, utawezaje kuwa na uhakika kuwa umeokaka?

Utakuwa na uhakika kuwa umeokaka kama maishaa yako itaanza kubadilika kuonyesha kuwa Mungu ameingia maishani mwa-ko.

Utakuwa na uhakika kuwa umeokaka kama baada ya miaka nyingi ungali unatembea na Kristo. Utakuwa na uhakika kuwa umeokaka kama unazaa matunda ya matendo mema.

(Tazama pia Yohana 5:10-13).

USALAMA WA MILELE

Ukianguka dhambini kesho au mwezi ujao, inawezekana kupoeteza zawadi yako ya uzima wa milele. Bibilia inasema :

kwa mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu. Na kila kuhani husimama kula siku akifanya ibada, na kutoa dhabibu zile zile mara nyingi ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi. Lakini ni huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi. Lakini ni huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele (yaliyopita, yaliopi na yajayo). Alifeti mkono wa kiume wa mungu.. maana kwa toleo moja amewakamilisja hata milele hao wanotakaswa. Waebrania 10:10-12, 14

Kulingana na Bibilia, kwa dhambi zipi ndiyo Yesu alilipa alipofariki?

- Dhambi zako zilizopita.
- Dhambi zako za kale na za sasa.
- Dhambi zako zote mile zilizopita, ziliopo na zijazo.
- Kulingana na mstrari huu, mara ngapi wewe utakaswa (wekwa mtakatifu) kupita kifo cha Yesu Kristo?
- Mara moja kwa Mara moja kila wakati una-kiri dhambo zako na kuomba msamaha.
- Mara moja kwa mwezi. Mara moja kwa zote.

USALAMA WA MILELE: UMUHIMU WA UTAMATI WA KUFA KWA BWANA

Mtu hapotezi zawadi ya uzima wa milele kwa sababu ya dhambi zako hiyo ndiyo sababu kufa kwa Kristo... kulipa dhambi zako. Ni kwa sababa alifia dhambi zote milele – yaliyopita, yaliopo na yajayo – kuwa anaweza mara moja na kwa yote kutangaza wewe hunu hatia.. sio tu kwa dhambi za kale, bali kwa dhambi zako zote: yaliopita, yaliopo na yajayo! Kukataa kuamini hii ni kukataa kuamini injili yenye!

USALAMA WA MILELE: UTAMATI MUHIMU WA NEEMA

Baada ya kwamni Kristo unatakitana kutunza sheria za Mungu ili "Kusalia umeokoka . . .

Ungesema ukweli kuwa uzima wa milele ni kwa neema (zawadi ya Bure)

NDIYO NA

AU

Ingemaanisha kuwa wokovu wako wategemea watendo ya sheria?

□ □

Kwa hivyo, mtu akikana wazi mafunzo ya bibilia kuhusu usalama wa milele kwa yule anayeamin, ni njia gain anayotumia kumfukia Mungu, kwa neema au kwa matendo ya sheria?

Mtu anaweza kudhubitishwa (okolewa) kupitia njia hii? (rejelea ukurasa 14:15). Bibilia inasemaje kuhusu kudhubitishwa kwa mtu? (Tazama Warumu 3:28 kupata usaidizi).

Ukurasa nyingine ya bibilia, Yesu alisema:

Kondoo wangu waisikia sauti yangu, nami nawajua, nao wanifuata nami nawaa uzima wa milele, wala hawata-potea kamwe, wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu. *Yohana 10:27-29*

Kupitia mstari, ni aina gain ya maisha Yesu alisema anapeana?

Ya muda Ya Masharti Ya milele

Kama ukweli ni wa milele jinsi Yesu alivyosema, inaweza kupotezwa?

Ndiyo Na

Katika mstari uliopewa hapo juu, nani Yesu alisema kuwa ali-kuwa mkuu kuliko wote?

Ni hali gain ya ukuu mtu anastahili kuwa nayo ilikuoka katika mkamato wa Mungu?

Wewe ni mkuu kuliko Mungu Baba?

Kuangaza mstari huu, kama umeamini injili ya wokovu, in-awezekana kufanya kitu ambacho matokeo yake ni ghadhabu ya milele ya Mungu?

(kuongezea maandiko mengine juu ya usalama wa milele: tazama , warumi 8:37-39, Waefeso 1:13-14, Yohana 6:37-40, Waebrania 13:5)

JE, TUTAENDELEA KUTENDA DHAMBI?

Ingawaje hakuna dhambi itakayo mnyang'anya anayeamin uzima wa milele tuliyopewa naye bure mara moja na kwa wote, dhambi ingawa inamatokeo ya kaburi kwa maisha tuliyonayo na maisha ijayo.

Kwanza, kuna matokeo ya kiasili ya dhambi.

Mtu annayelewa kupindukia anaweza kujiua mwenyewe au mtu asiyekuwa na hatia wakati wa ajili ya magari. Mtu anaye fanya usherati anaweza kupata ukimwi na baadaye kufa. Kumjua Kristo kama mwokozi kutamwokoa mtu kuingia jehanamu, lakini haitamwokoa mtu kwa matokeo ya kiasili ya dhambi au maisha ya ujinga. (tazama wagalatia 6:7-8, Yakobo 2:14-17)

Pili, kuna matokeo ya milele ya dhambi.

Kupokea tiketi ya bure kwenye tukio la mchezo ni dhamana mtu kuingia ugani, lakini si dhamana kwa mtu kukalia kiti cha mbele. Vivyo hivyo, kupokea zawadi ya bure maisha ya milele kupitia imani kwa Yesu Kristo ya mdhamini mtu kuingia ufalme wa mungu wa milele, lakini si dhamana kwa mtu kupewa nafsi ya juu kwenye ufalme wa Mungu wa milele, lakini si dhamana kwa mtu kupewa nafsi ya juu kwenye ufalme; nafasi yetu mbinguni na tuzu tupeazo kulingana na nafali inategemea maisha. (1 Wakontho 3: 11- 17, 9:24-27, Luka 19:11-27, 2 Wakontho 5:10-11) Wakati ambapo raha za dhambi kwa maisha haya huenda sasa zingine ikaonekana ya muhimu zaidi kuliko tumaini la mbali la thawabu zijazo mbinguni, maandiko intu-funzo ya kwamba wale ambaubadilisha "urithi" (thawabu yao ya usoni mbinguni) kwa maana anasa za dhambi siku moja watu wataombole za kwa ajili yao watakapoona thawabu kubwa mno walizowacha walipofuata anasa zao mbaya wakati wao ya mai-sha. (waebrania 12:14-17; Luka 19:11-27; Mathayo 25:14-30).


Tia mizizi katika imani yako

Katika siku shetani ataanza mashambulizi kwako ili aweze kujaribu kufinya chini imani yako katika kristo (1 petro 5:8, waefeso 6:16, Mathayo 13:3-23)

Baadhi ya malengo hasa ni:

1. Kupanda mbegu za shauku na kukataa tamaa ili akunyang'anye furah na uhakikishe kwa uzima wako wamilele.
2. Kukuongoza vibaya ili akuepushe kukua katika maarifa ya kweli na
3. Kukuzuia kushiriki imani yako kwa wengine ili kusimama wima dhdi ya mashambulizi yake.

Here are some tips on how to stand firm against his attack.



Ngao ya imani (waefeso 6:10-17)

1. Kwa vile injili ni jiwe kuu la pepmbe mwa imani ya mkristo, shetani mara moja ataanza kuweka mashambulizi yakekea kujaribu kukuchanganya juu ya ukweli wa injili ili upate kustahimili mashambulizi yake ambayo uko tayari kukabiliana nayo ana kwa ana, ni lazima uwe umetiwa mizizi barabara katika ukweli wa injili. Ilikufanya hivi jikakakmue sasa hivi kwamba utakisoma kijitabu hiki mara moja kwa siku kwa mwezi mzima. Usikome baada ya siku kumi au kumi na tano hata ukiwa umelikariri mawazoni. Na zaidi ya yote, usimruhusu shetani kukushusha moo kwa kukumbia eti unavyo vitu vya muhimu zaidi vya kufanya" Huu ni mfanano mzuri wa uongo wa shetani, usiamini (Mathayo 13:1-9, 19:23, 8:21-22; Luka 10: 38-42, 11:16-31, 14:16-20, Waefeso 5:16).

2. Usijaribu kupata uhakikisho wa uhusiano wako na kristo ama kukua katika ukweli wa kiroho kupertia kwa hisia za kigeni, ama sauti ndogo tulivu, ndanni ya kichwa chako, kile tunahisi katika miyo yetu sio mwongozo inayoweza kuanminika kwa ukweli wa kiroho kuliko kujaribu kuendesha mamia ya maili kurudi katika barabara za mashambani eti umeamini "hisia" zako? Bila shaka sivyo? Ilihali hivi ndivyo watu wengi kwa njia ya upumbavu kujaribu kuishib maisha yao ya ki Kristo.

3. Tutaweza kukua katika ukweli wa kiroho Mungu ameshatupatia chanzoo cha ukweli uliohakika na dhabiti. Inaitwa bibilia jaribu kusoma bibilia yako kila siku, anza wagalatia, inaongea juu ya Paulo kutetea injili na kutete injili na mafunzo ya Neema. Soma sura moja kila siku. Mpaka uweze kusoma kitabu chote (sura sita). Mara tano. Hii itachukua mwezi moja, mwezi ufuatao somo kitabu chote mara moja kwa siku hii itakuweka uwe thatbiti katika mafundisho mengi ya kimungu kwa imani ya mkristo ikizalisha aina ya msingi iliyomuhimu kwa kukuwa vizuri. Ki kristo.

Hisia huenda ikawa ni manong'onezano ya shetani.

Hisia
kutetemeka kwa ukukua
kiroho usiku moja, nguru
rumo za radi
hisia ya kutekerenywa



Basi imani, hanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa ne la Kristo.
Warumi 10:17

4. Mara ukishakuwa wima katika uelevu wako wa injili tafuta kanisa zuri. Kufanya hivi, uliza mchungaji vile mtu anawenza kwenda mbinguni, akisema ni kupertia kwishi maisha mazuri kutii amri kumi, ubatizo, kukiri, kuwa mwanachama wa kanisa, ama majibu mengine yasiyokuwa sahihi – geuka na utafute kanisa lengine kama mchungaji hajui hata injili, imani ya kimsingi mno ya imani ya mkristo, basi hata haelewii wala kujua kitu cha kwanza juu ya ukristo. Mbona ungependa kwenda kwa kanisa penye hata mchungaji hatafahamu hat jinsi watu wanaweza ingia mbinguni? Tafuta kanisa nzuri.

SHUKURU MUNGU KILA SIKU

Kulingana na bibilia, mambo mengi ya ajabu yalukotea wakati ulielewa injili na kumwamini kristo peke yake kama mwokozи wako.

- ◆ Ulipkoea msamaha wa dhambi zako zote ulizotenda.
(Warumii 5:1)
- ◆ Ulipokea uzima wa milele kama zawadi ya bure.
(Yohna 5:24, 10:28)
- ◆ Umehakikishiwa kuingia mbinguni. (Yohana 14:1-3)
- ◆ Alifanyika mwana wa Mungu. (Yohana 1:12)
- ◆ Unarafiki anayewe yale amabyo unapitia, na yuko karibu kukusaidia wakati wa mahitaji.
(Webrania 2:18, 4:15-16, Zaburi 68:5)

Katika Luka 17:11-19, Yesu alikada watu kumi wenye ukoma, tisa kati yao walienda njia yao ila kusimama na kumshukuru? Husifuta mfano ya watu tisa. Unaweza toak shukrani yako kwa Mungu kwa yale ambayo amekutendea kwa kuishi maisha yanayompen-deza kutii amri zake na kutembea kulingana na neon lake (Lk 7:40-43, Yohana 4:19, 14:21).

SHIRIKI INJILI

Wazia siku moja unatembea kando ya barabara, na kinanda ambacho kulikuwa kinachezwa katika gorofa la kumi kwa nyumba iliokatika gorofa moja mijini ilivunjika na kuanguka, na inaanguka upande wako bila maarifa yako. Mara ghafla, mtu ambaye hu-jawahi kukutana naye anakimbia kwako na kukusma toka njia ili akuokoe, badala yako ni yeye ndiye anaangukiwa na kile kinanda. Anapolala chini akifa, mkono wake unaotetetemeka unatoa barua mfukoni mwake. Je, utaituma? Bila shaka ndiyo?

Yesu, aliyekufa kukuokoa, ameacha aina hiyo ya barua na wewe. Hiyo barua inaitwa Injili. Na akawwambia, “enendeni ulimwen-guni mwote na mkaiburi injili kwa kila kiumbe” (Marko 16:15). Pia tazama 2 Wakorintho 5:18-20) Mathayo 28:18-20, matendo ya Mitume 1:8, Warumi 10:14-1) Je, unahiari kuichukua barua ambayo Yesu amekuwachia na kujaribu kufanya vile ambavyo ame-kuuliza?

Ikiwa unahirari kwa rahisi muulize rafiki yako au mwandani wako, “ Je, mtu yeyote ashakurejesha kutoka kwa biblia jinsi unavyowe-za, kuwa na hakika kuwa utaenda mbinguni ukifa? Wakisema “ha-pana” kirahisi “Je ninawenza? Watu wengi wanahiari kutaka kujua jinsi wanavyowenza kuwa na hiyo hakikisho. Ikiwa wanatamni chukua hatua na ushiri nao pamaja na kitabu hiki. Watafurahi mile!

JUU YA KIJITABU HIKI CHA INJILI

Wakati huu kuna aina mbalimbali ya habari ya “Injili” ambayo imeenea kote duniani. Yamepangwa kwanza mazungumzo ya wali ya kumtia nguvu mtenda dhambi mpotovu hadi : maonyo ya kumtia asiyemini hofu ili “ atubu dhambi zake” Haitishi, ana-yeamini na asiyemini wote wameachwa katika hali ya kukangan-yika. Hata kama injili imetangazwa dhahiri na barabara, msikilise lazima achague maneno ya mwinjilisti kupitia kwa gombo la injili bandia lililotangulia hapo wali ambacho tayari alikuwa ashalisikia na basi kushindwa, luelewa ujumbe unaoleta wokovu wa Yesu Kristo. Kutilia haya maanani, kitabu hiki cha Injili kiliandikwa sio tu kwa kufanوليwa na kueleza vipengele muhimu ya imani iokowayo kama vile. Kufanuua vitu vingi vya kibilia vyenye undani katika kijita kiki kifupi, rahisi kusom kilichukua karibu miaka tano na kurekebisha. Tunajua hakuna kijitabu kilichochapishwa leo kinachoashiria injili kwa uwazi au kwa uhakika.Ni ombi langu kuona kuwa kijitabu hiki cha injili kimepokea uenezi pakubwa. Makundi mengi y wakristor katika nchi za kigeni wamepewa lese-ni kuchapisha na kueneza kitabu cha injili katika nchi zao. Kupitia jitihada za makanisa na makundi ya kimishonari. Kijitabu hiki cha injili kimeshatafsiriwa kwa lugha muhimu za dunia. Kama wewe ni gwiji wa lugha ambayo bado haijonyeshwa kupitia tovuti letu, am unamjua yeyote, tunakukaribisha kuwasiliana nasi. Tuungane tufanye kazi pamoja kufanya kijitabu hiki kiwafikie watu kwa lugha zote.

KUHUSU MWANDISHI

Ron Shea alisoma chuo kikuu cha Villanova kwa miaka nne ya ufadhili na wa wanamaji wa Amerika. Baada ya kupata shaha-da la kwanza ya Electrical engineering, alihudumu kwa miaka nne kama afisa wa wanamaji, Kisha alihudhuria Dallas Theology Seminary, mahali alijihuisha kabisa na mafunzo ya agano jipya na ufanuzi, kutafsiri agano jipya lote kutoka lugha ya Ugiriki lilikuwa la kwanza. Alifuzu na Heslma baada ya miaka nne ya Masters of Theology Programme. Alijizidisha na kupata Doctor of Jurisprudence kutoka Chuo Kikuu cha California – Hastings College of Law, mahali alipata tuzo la Admiralty, Jurisprudence na Oral Argument. Amekuwa mchungaji wa makanisa huko New Orleans na San Francisco, na ndiye mwanzilishi na rais wa Clear Gospel Campaign.

Lengo la mtu ya milele hutegemea kile anachofanya na Yesu Kristo, kwa hivyo kufanya injili kuwa wazi ndiyo kitu muhimu sana ulimwenguni. Kitabu hiki kinatimiza lengo hilo. Mimi san asana nafurahi urahisi wake uliomakinika kulingana na kutubutu. Kijitabu hiki kitakuwa chombo chenye manufaa mikononi mwa yejote anayetegemea kuongaza wengine kwa Kristo.

Dr. Curtis Huston
President and Editor, Sword of the Lord

Ufafanuzi wa “toba” ni muhimu. Watu wengi hufikiria kuwa ni kugeuka kutoka kwa dhambi bali ni kubadilika akilini kuhusu jinsi wataokolewa. Umechangia pakubwa hapa. Sikuju kijitabu kingine kama chako ambacho kinafanya kazi nzuri ya ufanuzi ya injili.

Earl D. Radmacher, M.A., Th.D.
Chancellor and Professor of Systematic Theology, Western Seminary

Kwa siku Mara nyingi uinjilisti ukabishwa bila kuojali ukamilifu, inachamsha kuona mabo ya Injili katika utakatifu na nguvu jinsi inavyoangaziwa katika bibilia. Kwa wale wanaotaka uangazaji, bora wa Injili kwa matumizi kuongoza watu kwa kristo, kijitabu hiki kitakuwa jibu.

John F. Walvoord, Th.D.
Chancellor, Dallas Theological Seminary

Kampeni Bora ya Injili

Albanian	Igbo	Saraiki
Arabic	Indonesian	Sindhi
Bulgarian	Italian	Spanish
Burmese	Japanese	(Latin American)
Balochi	Kiswahili	Tagalog
Chinese (Traditional)	Polish	Tamil
Chinese (Simplified)	Punjabi, Western	Ugandan
English	Romanian	Ukraine
French	Russian	Urdu
German	Rwandan	Vietnamese

Kuhitaji kijitabu hiki cha Injili katika lugha tofauti au kutarakilisha faili za PDF kwa utazamo wa komputa na kuonyesha. Tafadhali tazama kurasa zetu za tovuti kwa :